

NATESEKA MUNGU WANGU

*Na: D.R.Kidaha
St.Gabriel Choir
01.06.2005*

Taratibu na Ibada

- 2(a) Adui zangu wanisakama, wadeni wangu waniandama,
(b) Siwezi mimi naangamia, naomba Baba uniokoe;
Ee Mungu uniokoe.

3(a) Jirani zangu wamenitenga, rafiki zangu wamekimbia,
(b) Hata ndugu zangu wamenitenga, hakuna anayenijali mimi;
Ee Mungu uniokoe.

4(a) Baridi joto vyanisakama, upepo mvua vyaniandama,
(b) Ninapeperuka kama majani, sina msaada naangamia;
Ee Mungu uniokoe.

5(a) Najiuliza maswali mengi, nikosa gani nililotenda,
(b) Hata niteseke kiasi hiki, Mungu nisamehe madhambi yangu;
Ee Mungu uniokoe.